TANGAZO LA SERIKALI Na. 316 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA NZERA CENTER YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Nzera Centre ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji la mpango wa urasimishaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 401578MS, 9713273KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS161° kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 405930MS, 9713273KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ52°MS kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 409186MS, 9714307KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Magharibi katika uelekeo wa KZ204°MG kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 405410MS, 9716863KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ57°MG kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 402961MS, 9720803KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS120°MG kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 400295MS, 9715126KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS125°MS kwa umbali wa kilomita kilomita 0.2 hadi ulipoanzia"

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*